

**Hituba ya Bwana Toshio Nagase, Mwakilishi Mkuu wa  
JICATanzania Office aliyotoa kwenye shughuli ya kupokea  
ripoti ya vijana waliorudi kutoka kwenye mafunzo chini ya  
program ya ABE Initiative – 6 Aprili, 2017**

**Mheshimiwa Mgeni wa Heshima, Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya  
Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ndugu Roxsana  
KIJAZI**

**Mheshimiwa Balozi wa Japan nchini Tanzania –Bwana Masaharu  
YOSHIDA**

**Washiriki wa ABE Initiative**

**Wageni Waalikwa**

**Mabibi na Mabwana**

**Habari za Asubuhi!!!**

Nina Furaha kubwa kuwakaribisha kwenye shughuli hii muhimu ya kupokea ripoti ya kundi la kwanza la wanafunzi waliorudi kutoka Japani kwenye mafunzo chini ya program ya ABE Initiative.

Hadi sasa, JICA imeshapeleka Japani wanafunzi 73 kuhudhuria mafunzo ya Shahada ya Uzamili (Masters' degree) chini ya mpango wa ABE Initiative. Suala hili limefanyika kwa ushirikiano mzuri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Kundi la kwanza lilikuwa na vijana wa kitanzania 29 ambao waliondoka nchini mwezi Septemba mwaka 2014.

Ninapenda kuwapongeza vijana wote waliorudi kwa kumaliza salama masomo yao na wote ambao walibahatika kufanya mazoezi katika kampuni za kijapani nchini Japan.

Kama mnafahamu, lengo la kutoa Shahada hii ya pili ni kuwaunga mkono vijana ambao wana mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ya viwanda katika Afrika. Programu hii inatoa nafasi kwa vijana wa kiafrika, wa kike na wa kiume kuweza kusoma shahada ya pili katika vyuo vikuu vya Japan kama wanafunzi wa kimataifa na pia kufanya mazoezi ya vitendo katika viwanda vya Kijapani kwa lengo la kuwajengea uwezo ili kuweza kushiriki katika nyanja mbalimbali. Mbali na hayo pia kupata ujuzi. Program hii inalenga kutoa wachapakazi ambao wanaweza kubaini na kuelewa jinsi jumuiya ya kijapani inavyofanya kazi.

JICA, tumekuwa tukipelewa vijana sio tu kutoka Serikalini bali pia kutoka katika sekta binafsi, kutoka vyuoni na hawa wanatoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Kulingana na yale waliyojifunza kule Japan, nina imani na ni mategemeo yangu kuwa hawa vijana watajenga daraja kati ya makampuni ya Kijapani na viwanda vya nchini Tanzania ambao pia wataboresha ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na Japan.

Zaidi ya hayo, kwa kutumia nafasi hii ya leo, vijana waliorudi watapata wasaa wa kuanzisha mawasiliano sio kwao wenyewe tu bali hata na wenye makampuni ya Kijapani ambao tuko nao hapa.

Leo hii, vijana 20 waliorudi wanatoka katika mashirika mbalimbali na watatueleza nini waliochosoma kule Japan pia watatueleza mipango yao ya baadae baada ya kupata mafunzo haya. Natumaini ripoti yao itavutia sana na tuwasikilize wanatwambia nini kati ya mambo hayo mawili.

Vijana mlilorudi,

Mnanikumbusha wakati mimi nilipokuwa mwanafunzi nchini Marekani wakati nasomea digirii yangu ya pili, wakati huo nilikuwa kijana bado, nilichokiona, na kusikia nikakihisi moyoni na kujifunza kutoka Marekani na nilikichukua kama mfano wa kuigwa kwenye nchi yangu ya Japan; na niliapa kuwa nitashiriki katika kuleta maendeleo ya nchi yangu baada ya

